**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**WILAYA YA UKEREWE**

**MTIHANI WA KIDATO CHA KWANZA**
**021 KISWAHILI**
**MUDA SAA 2:30 MWAKA: 2025**

**MAELEKEZO**

1. Mtihani huu unasehemu A,B na C zenye jumla ya maswali kumi **(10)**
2. Jibu maswali yote
3. Andika jina lako katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia
4. .Majibu yote yaandikwe kwa usafi na kwa uwekevu.

**SEHEMU A (ALAMA 15)**

**Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele i-x andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali.**

(i) Neno chachandu lina silabi ngapi?

A. Tatu C. Tano B. Nne D. Tisa

(ii) Mwanafunzi **hodari** anasoma. Neno lililo pigwa mstari ni aina gani ya neno?

A. Nomino C. Kivumishi

B. Kielezi D. Kiwakilishi

(iii) Ili mawasliano yawe mazuri wazungmzaji wanatakiwa kutumia.....

A. Lugha ya kiswahili C. Lugha fasaha

B. Lugha ya taifa D. Lugha asili

(iv) “nimemkuta hayupo hili ni kosa la:..

A. Maana C. Matamshi

B. Mantiki D. Muundo

(v) Wingi wa neno shule ni:-

A. Shuleni C. Vishule

B. Mashule D. Shule

(vi) Nahau inayosema “amevaa miwani” Inamaanisha nini?

A. Amependeza C. Amelewa

B. Ana makengeza D. haoni

(vii) “a,e,i,o,u, hizi ni :-

A. Irabu C. Konsonati

B. Silabi D. Sentensi

(viii) ...... ni neno kuanzia moja na hutoa ujumbe kamili.

A. Herufi C. Silabi

B. Sentensi D. Kosonati.

(ix) Tulicheza ngoma na kuimba usiku kucha. Katika sentensi hiii watenda ni nafsi ipi?

A. Ya tatu wingi C. Ya kwanza wingi B. Ya pili wingi D. Ya kwanza Umoja

(x) Neno lipi ni tofauti na mengine?

A. Sahibu C. mwandani

B. Ajuza D. mwenzi

**2.** Oanisha dhana zile zilizo katika sehemu **A** na zilizo katika sehemu **B**

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| (i) Nguvu inayotumika kutamka sehemu fulani ya neno.<br>(ii) Msomaji wa hadithi ndefu kusimulia kwa maneno machache.<br>(iii) Projecta, kipaza sauti kompyuta, simu, radio.<br>(iv) Hotuba, kampeni za kisiasa, Midahalo.<br>(v) Hupunguza ukali wa maneno. | A) Kiimbo<br>B) Mkazo<br>C) Tafsida<br>D) Tehama<br>E) Mazungumzo changamani<br>F) Msimuliaji<br>G) Ufupisho<br>H) Majadiliano |

**SEHEMU B (ALAMA 70)**

3. a) Amina aliwaomba wazazi wake wamnunulie kamusi ya kiswahili lakini wazazi wa Amina waliamini ununuzi wa kamusi ni upotevu wa fedha. Wewe kama rafiki wa Amina, washauri wazazi wa Amina kwa kuwaeleza hoja tano za umuhimu wa kumnunulia kamusi Amina.

b) Je,lugha ya kiswahili imepewa hadhi gani kimataifa? (taja hoja tano)

4. (a) Sentensi zifuatazo zina makosa, ziandike kwa usahihi

i) Nipatie fiatu fyangu tafasali
ii)Baba amenunua mbuzi
iii)Rehema amekwenda Ilinga
iv) Tulipomariza kula,tulirara
v)Nimekuelewapo vizuri

(b) Elezea maana ya lugha. Kisha na uelezee kwa mifano mifumo inayounda lugha.

5. Chunguza sentensi zifuatazo, kisha bainisha aina za maneno yaliounda sentensi hizo

i. Lo! Mwanafunzi nadhifu amefaulu mtihani
ii. Kokoto zile zimekusanywa na wanakijiji
iii. Yule amekwenda shuleni kwa miguu
iv. Mimi ninapenda kujifunza Kiswahili
v. Kijana huyu ni mtukutu sana

6. a)Taja mambo matano yakuzingatia katika kusoma kwa ufasaha

b) Umuhimu wa ufahamu katika maisha yake ya kila siku(hoja tano)

7. (a) Eleza maana ya kamusi.

(b) Taja aina tatu (3) za kamusi unazozifahamu.
(c) Eleza jinsi ya kutumia kamusi kupata maana ya maneno.

8. (a) Eleza maana ya muktadha wa mawasiliano.
(b) Taja muktadha mitatu (3) ya mawasiliano katika jamii.

(c)Eleza kanuni tatu (3) za mawasiliano bora katika jamii

9. (a) Tofautisha kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi.
(b) Toa mifano miwili (2) ya sentensi za lugha ya mazungumzo na miwili (2) ya lugha ya maandishi.

(c) Eleza faida tatu (3) za kuimudu lugha ya mazungumzo.

**SEHEMU C( ALAMA 15)**

10 Andika barua kwa mama yako umuombe nauli ya kwenda likizo mara tu utakapo maliza mitihani yako na kufunga shule .